

SHULE YA SEKONDARI OLD KOROGWE,
S. L. P 267,
KOROGWE.
14/12/2020.

KUMB. Na. OKSS/JI/Vol. 1/2021/1

JINA.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI OLD KOROGWE, WILAYA
YA KOROGWE MJI, MKOA WA TANGA MWAKA 2021**

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule ya Sekondari Old Korogwe mwaka 2021. Shule ipo umbali wa km 3, toka Manundu Korogwe. Usafiri wa bajaji kutoka Manundu Korogwe au Stand Old Korogwe unapatikana.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shule tarehe hiyo. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Sare za shule hii kwa wavulana ni suruali mbili (2) za kijani zenye rinda mbili na mifuko mitatu. Hakikisha suruali hazibani, upana wa miguu usipungue inchi 16. (kitambaa kimeambatanishwa).

Sare za wasichana ni sketi mbili za kijani, mshono rinda boksi na ufito mweupe. Zishonwe vizuri kwa urefu unaovuka magoti. Wanafunzi wanaovaa Hijab watapata maelekezo shuleni.

Wanafunzi wasiovaa Hijabu, kwa wavulana na wasichana kila mmoja awe na shati mbili nyeupe za mikono mifupi, viatu ni vyeusi vyenye kisigino kifupi na vya kufunga kwa kamba kwa wavulana na wasichana.

2. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI;

- I. Medical Examination Form,
Ijazwe na mganga mkuu wa hopsitali ya selikali na iwasilishwe kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi awasilipo shuleni.
- II. Vifaa vya michezo; Kila mwanafuzi aje na nguo za michezo (Track suit ya blue au T-shirt ya blue na bukta)
- III. Vifaa vya usafi; Kila mwanafunzi anatikwa kuja na ufagio (01) wa chelewa, ndoo moja (01) ya lita 10 kwa ajili ya usafi,
- IV. Vifaa vya darasani; Kila mwanafuzi anatakiwa kuwa na madaftari aina ya "counter book" kuanzia quire 2 kwa masomo yote kwa ajili ya kumbukumbu za kila somo na kwa kila somo awe na daftari la mazoezi. Mwanafunzi anatakiwa kuja na ream moja ya karatasi (photocopy paper) kwa ajili ya mitihani ya ndani na majaribio. Mwanafunzi anashauriwa kuwa na dictionary (kamusi ya kiingereza) kwa ajili ya kukurahisisha ujifunzaji.
- V. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;
(a) Wizi (b) uasherati (c) ubakaji (d) ulevi (e) kupigana au kupiga (f) kuharibu kwa makusudi mali ya umma (g) kudharau bendera ya taifa (h) kuoa au kuolewa (i) kutoa mimba (j) kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu (k) kukataa adhabu kwa makusudi (l) kuwa simu ya mkononi. Mwanafunzi anatakiwa kudumisha NIDHAMU muda wote awapo shuleni na hata nje ya shule.

" NO SUCCESS WITHOUT EFFORT "
HAKUNA MAFANIKIO BILA JITHADA

KARIBU SANA OLD KOROGWE SEKONDARI

.....
S. J. KUSSAGA
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
OLD KOROGWE SECONDARY SCHOOL

MEDICAL FORM

(To be completed by the Medical Officer in respect to form I entrants).

Pupil's full name
Age Year Sex

Stool Examination

Urine examination

T.B Test

Hearing

Sigh

Abdomen

Spleen

Pregnant test

Any other abnormalities e.g physical defects chronic family diseases cts

.....
.....
.....

I certify that the above pupil is fit until for admission into a boarding / Day Secondary School

Signature Designation

Station Date